# AZIMIO LA SHULE SALAMA

**Athari za vita kwa elimu ni changamoto kubwa kwa binadamu, maendeleo na jamii kwa ujumla. Kote duniani, Shule na Vyuo Vikuu vimeshambuliwa kwa mabomu, na kuteketezwa, huku wanafunzi, waalimu na wasomi wakiuawa, kujeruhiwa, kutekwa au kuzuiliwa. Majengo ya elimu yametumika na wanajeshi au makundi ya wapiganaji kama kambi za kijeshi au kama maeneo ya kuwazuilia wafungwa. Hatua kama hizo zimewaweka wanafunzi na wafanyakazi katika sekta ya elimu katika hatari kubwa. Pia imewanyima idadi kubwa ya watoto na wanafunzi haki ya kupata elimu na kuzinyima jamii msingi wa kujenga mustakabali wao. Katika nchi nyingi, vita vinaendelea kuharibu sio tu majengo ya shule bali pia matumaini na matarajio ya kizazi kizima cha watoto.**

Elimu imevurugwa kwa njia kadhaa ikiwa ni pamoja na kuharibiwa kwa majengo ya shule, unyanyasaji wa wanafunzi na wafanyakazi katika sekta hii. Mashambulizi, na vitisho vya kushambuliwa, husababisha madhara ya muda mrefu kwa watu binafsi na jamii. Masomo yaweza kukatizwa, upatikanaji wa elimu unakuwa mgumu sana, utendaji kazi wa taasisi za elimu unaweza kuvurugwa, au wahudumu wa taasisi hizo na wanafunzi wao kukosa kufika, kwa kuhofia usalama wao. Mashambulizi ya shule na vyuo vikuu hukuza hali ya kutovumiliana na kutengwa kwa baadhi ya watu katika jamii – mara nyingi ukiendeleza ubaguzi wa kijinsia. Kwa mfano kwa kuzuia elimu ya wasichana, na kuendeleza migogoro kati ya jamii fulani, kuzuia kutangamana kwa utamaduni, na kuwanyima baadhi ya watu uhuru wa usomi au kushirikiana na wengine. Pale shule na taasisi nyingine za elimu zinapotumika kwa shughuli za kijeshi hali hii huongeza hatari ya watoto kusajiliwa kama wapiganaji, au kuwaweka katika hatari ya kubakwa au kutumika vibaya. Kwa msingi hali hii inazidisha uwezekano wa taasisi hizo kushambuliwa.

Kwa kulinganisha, elimu inaweza kusaidia kuwalinda watoto na vijana kutokana na vifo, kujeruhiwa au kutumika vibaya; inaweza kupunguza athari za kisaikolojia zinazotokana na mizozo ya kivita kwa kutoa utaratibu na utulivu na kutoa fursa ya kupatikana kwa huduma nyingine muhimu. Elimu inayotolewa kwa kuzingatia misingi ya kuepukana na mizozo hujiepusha na kusababisha mizozo na huchangia kuwepo amani. Elimu ni muhimu katika maendeleo na huwezesha kuwepo haki kamilifu za binadamu na uhuru. Tutajitahidi kuhakikisha kwamba shule na taasisi nyingine za elimu ni maeneo salama.

Tunakaribisha juhudi za mataifa binafsi kukuza na kulinda haki ya kupata elimu na kuwezesha kuendelea kwa elimu wakati wa vita au mzozo. Kuwepo kwa masomo katika wakati wa vita au mzozo ni muhimu kwa kuwa kunatoa fursa ya ubadilishanaji wa habari ambayo inaweza kusaidia kuokoa maisha pamoja na kutoa ushauri wa hatari ambayo huenda ikaikabili jamii fulani wakati wa vita.

Tunapongeza kazi inayofanywa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linalohusika na masuala ya watoto na vita na kutambua umuhimu wa utaratibu wa ufuatiliaji na kuripotiwa kwa visa vya ukiukwaji mkubwa dhidi ya watoto katika vita. Tunasisitiza umuhimu wa azimio la Baraza la Usalama la 1998 (2011), na 2143 (2014) ambalo, pamoja na mambo mengine, linahimiza makundi yote katika mzozo wa kivita kujiepusha na vitendo ambavyo vitawazuia watoto kupata elimu, tunawahimiza nchi wanachama kuzingatia hatua madhubuti kuzuia wanajeshi au wapiganaji kutumia majengo ya shule hii ikiwa ni ukiukaji mkubwa wa sheria za kimataifa.

Tumefurahishwa na kuratibishwa kwa *Mwongozo wa kulinda shule na vyuo vikuu kutokana na matumizi ya kijeshi wakati wa vita*. Mwongozo huu sio wa kisheria, na sio wa kushurutisha lakini ni wa hiari na hautaathiri sheria za kimataifa zilizopo. Umeandikwa kwa kuzingatia mifano bora iliyopo kwa sasa na unalenga kutoa mwelekeo ambao utasaidia kupunguza athari za vita katika elimu. Tunakaribisha juhudi za kusambaza Mwongozo huu na kuhimiza utekelezwaji miongoni mwa wanajeshi, makundi yenye silaha, na wadau wengine wanaohusika.

Tunasisitiza umuhimu, kwa hali zote, heshima kamili kwa sheria husika za kimataifa, ikiwa ni pamoja na haja ya kuzingatia masharti ya kuangamiza hali ya ukiukwaji wa sheria.

Tunatambua haki ya kila mtu kupata elimu na mchango wa elimu katika kukuza uelewa, uvumilivu na urafiki kati ya mataifa yote; yaliyojitolea kuimarisha kwa vitendo juhudi za kulinda raia katika vita, hasa kuwalinda watoto na vijana; nia ikiwa kufanya kazi kwa pamoja ili kuwezesha kuwepo usalama shuleni kwa wote; tunaidhinisha *Mwongozo wa kulinda shule na vyuo vikuu kutokana na matumizi ya kijeshi wakati wa vita*, na:

- Tutatumia Mwongozo wa kulinda shule na kuuiainisha na sera na mifumo inayotumika katika nchi husika kama inavyowezekana na katika njia inayofaa;
- Tutachukua kila hatua katika ngazi ya kitaifa kukusanya takwimu (data) za kuaminika kuhusu mashambulizi dhidi ya shule na taasisi nyingine za elimu, waathirika wa mashambulizi, na juu ya wanajeshi kutumia maeneo hayo wakati wa vita, ikiwa ni pamoja na kutumia njia ya ufuatiliaji na kuripotiwa kwa taarifa kwa utaratibu; kuwezesha kukusanywa kwa takwimu, na kutoa msaada kwa wathirika, kwa namna isiyobaguwa;
- Kuchunguza madai ya ukiukwaji wa sheria husika za kitaifa na kimataifa na, ikiwa inafaa, kihalali kuwashtaki wahusika;
- Kuendeleza, kukumbatia na kutumia njia ambazo zinatambua na kuzingatia utata wa migogoro wakati wa kutoa mafunzo katika programu za kimataifa za kibinadamu na maendeleo, na katika daraja ya kitaifa;
- Tutahakikisha kuwepo kwa elimu wakati wa vita, kusaidia kuanzishwa upya kwa taasisi za elimu, na pale ambapo tunaweza, kutoa fursa na kuwezesha ushirikiano wa kitaifa na usaidizi kwa programu zinazofanya kazi kuzuia mashambulizi au kutoa msaada kwa waathiriwa wakati wa mashambulizi dhidi ya taasasi za elimu, ikiwemo pamoja na kutekelezwa kwa azimio hili;
- Kusaidia juhudi za Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linalohusika na masuala ya watoto na vita, na ofisi ya Mwakilishi Maalum wa Katibu – Mkuu wa masuala ya Watoto na Migogoro ya kivita na vyombo vingine vya Shirika la Umoja wa Mataifa, na mashirika ya kijamii; na
- Kuandaa mikutano ya kila mara, na kuwaalika waakilishi wa mashirika ya kimataifa na kijamii yanayohusika na masuala haya, ili kuweza kuangalia upya utekelezaji wa azimio hili na matumizi ya *Mwongozo wa kulinda shule na vyuo vikuu kutokana na matumizi ya kijeshi wakati wa vita*.